**MKUTANO WA 35 WA KAWAIDA WA JUKWAA LA MPANGO WA KUJITATHMINI AFRIKA LA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA AFRIKA**

**RASIMU YA TAARIFA**

**TAREHE: 13 Februari 2026**
**MUDA: Saa 4:00 asbh – 8:00 mchana**
**UKUMBI: Medium Conference Hall, makao makuu ya UMOJA WA AFRIKA**
**Addis Ababa, Jamhuri ya Shirikisho ya Kidemokrasia ya Ethiopia**

1. Mkutano wa 35 wa Kawaida wa Jukwaa la Mpango wa Kujitathmini la Afrika la Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika (Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali) ulifanyika tarehe 13 Februari 2026,mjini Addis Ababa, Ethiopia, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda na Mwenyekiti wa Jukwaa la Mpango wa Kujitathmini Afrika la Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika (Jukwaa la APR), aliyewakilishwa na Mheshimiwa Meja Mstaafu. Jessica Rose Epel Alupo, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Uganda.

2. Wakuu wa Nchi na Serikali wafuatao walihudhuria Mkutano huo:

   1. Mhe. João Manuel Gonçalves Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika;
   2. Mhe. Duma Boko, Rais wa Jamhuri ya Botswana;
   3. Mhe.. Évariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi;
   4. Mhe. Faustin Archange Touadera, Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kati;
   5. Mhe. Azali Assoumani, Rais wa Muungano wa Comoro;
   6. Mhe. Ismail Omar Guelleh, Rais wa Jamhuri ya Djibouti;
   7. Mhe. Taye Atske Selassie, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho ya Kidemokrasia ya Ethiopia;
   8. Mhe. Brice Clotaire Oligui Nguema, Rais wa Jamhuri ya Gabon;
   9. Mhe. John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana;
   10. Mhe. Daniel Chapo, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji;
   11. Mhe. Netumbo Nandi-Ndaitwah, Rais wa Jamhuri ya Namibia;
   12. Mhe. Julius Maada BIO, Rais wa Jamhuri ya Sierra Leone;;

13. Mhe.. Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia;
14. Mhe. Emmerson Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe
15. Mhe. Américo d'Oliveira dos Ramos, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya São Tomé na Príncipe;
16. Mhe. Muhammad B.S. Jallow, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Gambia;
17. Mhe. Sebastien Pillay, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Shelisheli;
18. Mhe. Meja Mstaafu Jessica Rose Epel Alupo, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Uganda
19. Mhe. Sifi Ghrieb, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria;
20. Mhe. Dkt Mostafa Madbouly, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri;
21. Mhe. Jaji Nthomeng Majara, Naibu Waziri Mkuu wa Ufalme wa Lesotho.

3. Nchi Wanachama Wafuatao wa APRM zilizoshiriki ziliwakilishwa na Waheshimiwa Mawaziri na Maafisa wenye dhamana ya APRM pamoja na Maafisa Waandamizi wa Serikali: Jamhuri ya Benin, Jamhuri ya Cameroon, Jamhuri ya Chad, Jamhuri ya Congo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jamhuri ya Guinea ya Ikweta, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Liberia, Jamhuri ya Malawi, Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania, Jamhuri ya Mauritius, Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria, Jamhuri ya Rwanda, Jamhuri ya Sao Tome na Principe, Jamhuri ya Senegal, Jamhuri ya Sierra Leone, Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia, Jamhuri ya Afrika Kusini, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Togo, Jamhuri ya Tunisia, Jamhuri ya Zambia

4. Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Mheshimiwa Mahamoud Ali Youssouf, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika; Mheshimiwa Balozi Selma Malika Haddadi, Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni; Makamishna wa Umoja wa Afrika; Mheshimiwa Balozi Aly El-Hefny, Mwenyekiti wa Jopo la Kujitathmini Afrika (APR) la Watu Mashuhuri; Mheshimiwa Balozi Aly El-Hefny Ali Ahmed Araita, Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Watu Mashuhuri la APR; Wajumbe wa Jopo la Watu Mashuhuri la APR; Mhe. Balozi Marie-Antoinette Rose-Quatre, Afisa Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya Bara ya APRM; Mhe. Balozi Ashraf Rashed, Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Bara ya APRM ya Mabaraza ya Uongozi ya Kitaifa; Bw. Mohamed Sheriff, Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu ya Sekretarieti za Kitaifa za APRM; Wakuu wa Vyombo vya Kitaifa vya APRM; Wakuu wa Jukwaa la Mpango wa Utawala wa Afrika (AGA); Maafisa Wakuu wa Jumuiya za Kiuchumi za Kanda/Mifumo ya Kikanda; Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa; Washirika wa

APRM na Wafanyakazi Waandamizi wa Umoja wa Afrika.

5. Wakati wa sherehe ya ufunguzi, Mhe. Abiy Ahmed Ali, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Shirikisho ya Kidemokrasia ya Ethiopia, alitoa hotuba ya kumkaribisha. Mhe. Balozi Marie-Antoinette Rose-Quatre, Afisa Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya Bara ya APRM na Mhe. Balozi Aly El-Hefny, Mwenyekiti wa Jopo la Kujitathmini la Afrika la Watu Mashuhuri, kutoa hotuba wakati sherehe ya ufunguzi,

6. Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia imekuwa Nchi ya 45 Mwanachama wa APRM. Mkutano huo ulimpongeza Mhe. Hassan Sheikh Mohamud kwa hekima na uamuzi wa ujasiri wa kujiunga na APRM, chombo kikuu cha Umoja wa Afrika kilichoundwa ndani ya bara kwa ajili ya kukuza utawala bora barani. Mkutano huo ulimhimiza Mheshimiwa kufanya mapitio ya msingi mapema iwezekanavyo ili kuonyesha maana halisi ya kujiunga.

7. Katika hotuba yake ya kujiunga, iliyotolewa kwa niaba ya Mheshimiwa Hassan Sheikh Mohamud, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia, Mheshimiwa Abdisalam Abdi Ali, Waziri wa Uhusiano na Ushirikiano wa Kimataifa, alijikita kwenye Nguzo tatu (3) ambazo serikali ya Somalia inazipa kipaumbele ili kukuza demokrasia na utawala bora: (i). Kuimarisha taasisi za kidemokrasia na michakato jumuishi ya kufanya maamuzi; (ii) Kukuza Utawala wa Sheria na Haki za Binadamu; na (iii) Kukuza Uhimilivu wa Kiuchumi na Ushirikiano wa Kimkakati

8. Mkutano wa Wakuu wa Nchi ulitaarifiwa kwamba Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia itasaini mkataba wa makubaliano kuhusu kujiunga na mpango huo kesho.

9. Mkutano huo ulizihimiza Nchi zote Wanachama wa AU ambazo bado hazijajiunga na APRM kujiunga na mpango huo na zile ambazo zimejiunga lakini hazijafanya Mapitio ya Kwanza ya Nchi ya APRM kufanya hivyo. Mkutano huo pia ulizitaka Nchi Wanachama ambazo zimefanya mapitio kuwasilisha Ripoti zao za Maendeleo kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji

10. Mkutano huo ulifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Sifi Ghrieb, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa niaba ya Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Jukwaa la Wakuu wa Nchi na Serikali la APR. Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mheshimiwa Sifi Ghrieb, alirudia wito wake kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo bado hazijajiunga na APRM kufanya hivyo, ili zote ziwe wanachama kulingana na maagizo ya Mkutano Mkuu wa AU. Alizihimiza zaidi Nchi Wanachama wa APRM ambazo bado hazijafanya mapitio ya nchi kuzingatia kufanya hivyo ili kuimarisha utawala bora katika ngazi za kitaifa na bara.

11. Mheshimiwa Sifi Ghrieb alizipongeza Liberia, Senegal, Togo, na Djibouti kwa kulipa madeni yao kwa APRM na kuzitaka Nchi zingine Wanachama kufuata mfano huo, ikiwa ni pamoja na kupitia utoaji wa michango ya hiari, kama ilivyoonyeshwa na Algeria. Pia

alimwomba Mwenyekiti Mpya wa Jukwaa la APR kuendelea kuwahimiza wenzake kulipa madeni kulingana na uwezo wao wa kifedha. Alisisitiza kwamba vitendo hivyo vinaonyesha umiliki halisi wa APRM na Nchi Wanachama.

12. Mkutano wa Wakuu wa Nchi uliidhinisha Troika mpya ya Jukwaa la Wakuu wa Nchi na Serikali la APR kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya APR kwa mujibu wa Ibara ya 11 (2) (3) ya Mkataba wa APRM. Troika mpya ya APRM imeundwa kama ifuatavyo:

   - Mwenyekiti: Jamhuri ya Uganda, inayowakilisha Afrika Mashariki
   - Mwenyekiti anayemaliza muda wake: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, inayowakilisha Afrika Kaskazini
   - Mwenyekiti mpya kwa kipindi cha 2028 - 2030: Jamhuri ya Burundi, inayowakilisha Afrika ya Kati.

13. Mhe. Sifi Ghrieb, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria anayemwakilisha, Mhe. Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mwenyekiti anayemaliza muda wa Jukwaa la Wakuu wa Nchi na Serikali la APR, alikabidhi rasmi Uenyekiti wa APRM kwa Mhe. Meja (Mstaafu) Jessica Rose Alupo Epel, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Uganda, akimwakilisha Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda.

14. Katika taarifa yake ya kukubali, Mheshimiwa Meja (Mstaafu) Jessica Rose Alupo Epel alikumbusha kwamba Uganda ilikuwa miongoni mwa wanachama waanzilishi wa APRM, jambo ambalo linaipa nchi jukumu la kihistoria la kuchangia katika utekelezaji wa malengo na mamlaka ya Mpango huo. Pia alikumbusha, kwa shauku, Mkutano wa 2016 wa Jukwaa la APR, ambao ulibaini vikwazo 13 vinavyozuia maendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika na kuzihimiza Nchi Wanachama kufanya mapitio yaliyolengwa ili kuvishughulikia, hasa katika ujumuishaji wa soko.

15. Makamu wa Rais alisisitiza zaidi kwamba kipindi cha uongozi wa Uganda kitazingatia kaulimbiu "Kushughulikia vikwazo vinavyozuia maendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika kupitia utawala bora." Alilifahamisha Jukwaa kwamba Rais amedhamiria kuhakikisha utekelezwaji wa Shirika la Ukadiriaji wa Mikopo la Afrika; Uganda inaandaa Mkutano wa Usimamizi wa Uhamiaji Afrika; mwenyeji wa Mazungumzo ya Vyama vya Siasa kuhusu Demokrasia na Utawala Bora; na kuitishwa kwa Jukwaa la Nne la Ushirikiano wa Kusini-Kusini na Pembetatu mjini Algiers, Algeria. Alimalizia kwa kuzihimiza Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo bado hazijajiunga na Mpango huo kufanya hivyo, na zile ambazo tayari ni wanachama kuendelea kutoa michango ya hiari kwa APRM.

16. Mkutano huo ulizingatia na kupitia ripoti zifuatazo zilizofanyiwa mapitio:

i. Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya Ghana kuhusu Usimamizi wa Makampuni kama Kichocheo cha Utekelezaji wa AfCFTA katika Jamhuri ya Ghana;

ii. Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya Zimbabwe kuhusu Utawala na Usimamizi wa Uchumi;

iii. Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya São Tomé na Príncipe kuhusu Utalii kama kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni.

17.Kutokana na kutopatikana kwa Mhe. Julius Maada BIO, Rais wa Jamhuri ya Sierra Leone, na Mhe. Faure Essozimna Gnassingbé, Rais wa Baraza la Togo, Jukwaa lilikubali kuahirisha mapitio ya Ripoti ya Mapitio ya Nchi ya Kizazi cha Pili ya Jamhuri ya Sierra Leone na Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Togo kuhusu Uhimilivu wa Mijini: Majanga, Hatari na Hatua za Kukabiliana na hadi mkutano ujao wa Jukwaa la APR.

18.Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya Ghana iliwasilishwa na Mheshimiwa Balozi Aly El-Hefny, Mjumbe Kiongozi wa Jopo la Ghana. Katika majibu yake, Mheshimiwa John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana, alitambua uchunguzi, matokeo na mapendekezo ya Ripoti ya Mapitio Lengwa kuhusu "Usimamizi wa Makampuni kama Kichocheo cha Utekelezaji wa AfCFTA katika Jamhuri ya Ghana.

19.Rais Mahama alielezea mageuzi ya kisheria na sera yaliyofanywa ili kushughulikia mapendekezo hayo, akisisitiza kwamba mafanikio ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika yanategemea taasisi imara, uongozi wa kimaadili, uhakika wa udhibiti, na utendaji wa biashara ulio wazi. Alisisitiza kwamba usimamizi wa makampuni ni kichocheo cha kimkakati cha tija, ubunifu, upatikanaji wa fedha, na biashara ya mipakani.

i. Ghana imetekeleza mageuzi makubwa, ikiwa ni pamoja na Kanuni ya Kitaifa ya Usimamizi wa Makampuni na kuimarisha mifumo ya utawala wa fedha, biashara, na sekta ya umma. Serikali inaimarisha uwezo na uratibu wa taasisi muhimu za udhibiti—kama vile Benki ya Ghana, Tume ya Dhamana na Ubadilishanaji Fedha, Kituo cha Kukuza Uwekezaji cha Ghana, na Ofisi ya Msajili wa Makampuni—ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa viwango vya usimamizi wa makampuni.

ii. Sheria ya Makampuni, 2019, inaimarisha ubainishaji wa umiliki wenye manufaa, ripoti za kifedha, ukaguzi, na adhau kwa kutofuata sheria, kwa utekelezaji kamili ili kulinda wawekezaji, wafanyakazi, na maslahi ya umma. Ghana itaendelea kuoanisha mfumo wake wa usimamizi wa makampuni na mbinu bora za kimataifa kupitia ushirikishwaji wa wadau na kuendeleza Mpango wake wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Biashara na Haki za Binadamu ili kukuza mwenendo wa biashara unaowajibika na uwajibikaji wa kitaasisi.

iii. Ghana pia inawezesha Biashara Ndogo, Ndogo na za Kati na kutumia miundombinu ya umma ya kidijitali—ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Malipo na Makazi wa Afrika, ushirikiano wa malipo ya pesa kwa njia ya simu, na biashara isiyotumia karatasi—ili kupunguza

gharama ya biashara ya mipakani. Nchi bado imejitolea katika kurahisisha biashara, mageuzi ya forodha, na ujumuishaji wa kikanda, ikifanya kazi kwa karibu na ECOWAS na taasisi za bara ili kukuza usafirishaji huru wa bidhaa na watu.

iv. Zaidi ya hayo, Ghana imeunga mkono uidhinishaji wa makampuni 19 ili kufikia viwango vya AfCFTA chini ya Mpango wa Biashara Unaoongozwa, kuwezesha upatikanaji uliopanuliwa wa masoko ya bara na kuonyesha faida za vitendo za utawala ulioimarishwa na ujenzi wa uwezo.

20. Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya Zimbabwe iliwasilishwa na Balozi Aly El-Hefny, Mjumbe Kiongozi wa Jopo la Zimbabwe. Katika majibu yake, Mheshimiwa Emmerson Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, alitambua uchunguzi, matokeo na mapendekezo ya Ripoti ya Mapitio Lengwa kuhusu Utawala na Usimamizi wa Uchumi.

Rais Mnangagwa alielezea hatua zinazolenga kuimarisha utawala na usimamizi wa uchumi nchini Zimbabwe. Alibainisha masuala yafuatayo:

i. Zimbabwe imefanya mageuzi makubwa yanayolenga kuimarisha utawala wa kiuchumi, nidhamu ya fedha na uwajibikaji wa sekta ya umma, sambamba na Vifungu vya 12 na 13 vya Katiba ya Zimbabwe.

ii. Licha ya athari mbaya za hatua za kulazimisha za upande mmoja zilizowekwa katika miongo miwili iliyopita, ambazo zimezuia mtiririko wa uwekezaji, upatikanaji wa mikopo, uhamisho wa teknolojia na utendaji mpana wa kiuchumi, nchi inabaki imara katika kuendeleza maendeleo endelevu.

iii. Rais Mnangagwa alitoa shukrani kwa mshikamano wa SADC na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika katika kutoa wito wa kuondolewa bila masharti kwa hatua hizi.

iv. Serikali inaharakisha uboreshaji, viwanda, na ukuaji jumuishi kupitia mipango kama vile Mfumo wa Elimu 5.0 Unaotegemea Urithi, mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma, mifumo iliyoimarishwa ya kupambana na utakatishaji fedha, uwezeshaji wa sekta ya madini, na sera za kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni chini ya ZIDA.

v. Rais anathibitisha tena kujitolea kwake kusikoyumba kwa APRM kama jukwaa la mshikamano wa Afrika, kujifunza kwa pamoja na uwajibikaji wa pande zote, na anaahidi kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya Mapitio katika kutafuta uwazi, ujumuishaji na maendeleo endelevu kwa manufaa ya watu wa Zimbabwe.

21. Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya São Tomé na Príncipe iliwasilishwa na Balozi Ali Ahmed Araita, Mjumbe Kiongozi wa APRM wa São Tomé na Príncipe.

i. Katika jibu lake, Mheshimiwa Américo d'Oliveira dos Ramos, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya São Tomé na Príncipe, alikiri kuridhika matokeo ya Ripoti ya Mapitio Lengwa kuhusu Utalii kama kichocheo cha maendeleo ya Kiuchumi, kijamii na kitamaduni nchini São Tomé na Príncipe

ii. Waziri Mkuu dos Ramos alibainisha kwamba tangu mapitio yao ya mwisho, serikali imeanzisha na kutekeleza mageuzi. Haya ni pamoja na: kuweka kipaumbele cha uwazi, uwajibikaji, na ubadilishanaji wa kidijitali; upatikanaji wa haki ili kupambana na rushwa; juhudi zinazolenga kuleta utulivu wa uchumi na kuboresha mazingira ya biashara, kuzingatia uchumi wa bluu na utalii endelevu; utalii unaothamini mseto na kulinda utamaduni.

iii. Licha ya juhudi hizi, changamoto za mabadiliko ya tabianchi zinaendelea, na tunatarajia kuendelea na msaadai wa APRM katika kuimarisha uhimilivu na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko. Utekelezaji mzuri wa mapendekezo ya Mapitio Lengwa—kupitia mgao wa kutosha wa rasilimali na ushirikiano ulioimarishwa kati ya APRM na washirika wake wa kimkakati—ni muhimu, kwani utekelezaji unabaki kuwa muhimu kwa majukumu ya APRM.

iv. São Tomé na Príncipe inathibitisha uzingatiaji wake kamili wa kanuni za APRM, ambazo zinawaweka watu katikati ya utawala na maendeleo endelevu.

22. Mkutano huo uliwapongeza Rais Bio, Rais Gnassingbé, Rais Mahama, Rais Mnangagwa, na Waziri Mkuu dos Ramos kwa kukamilika kwa mafanikio kwa michakato yao ya mapitio na kuwatia moyo kuchukua hatua zinazohitajika katika kuandaa Programu za Kitaifa za Utekelezaji (NPoA) ili kutekeleza matokeo na mapendekezo ya ripoti zao. Mkutano huo pia ulizihimiza nchi hizo kuhakikisha kwamba NPoA zao zinaendana na Ajenda ya AU ya 2063, hususani Mpango wake wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka 10.

23. Mkutano huo ulielezea kuridhika kwake na Wajumbe wa Jopo la APR kwa uongozi wao wa mfano katika kufanya Mapitio ya Nchi ya Kizazi cha Pili ya Sierra Leone na Mapitio Lengwa ya Togo, Ghana, Zimbabwe, na São Tomé na Príncipe

24. Mhe. Daniel Francisco Chapo, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, aliwasilisha Ripoti ya Maendeleo kuhusu utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Utekelezaji ya Msumbiji, inayotokana na mapitio ya Kizazi cha Pili cha nchi hiyo yanayozingatia Nguzo nne (4): Demokrasia na Utawala wa Kisiasa; Utawala na Usimamizi wa Kiuchumi; Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi; na Utawala wa Kampuni. Rais Chapo alisisitiza ujumuishaji wa Chama cha Renamo kama mafanikio makubwa kuelekea utekelezaji wa utawala wa kisiasa. Mipango ya kufanya huduma za sekta ya umma kuwa za kidijitali inaendelea.

25. Mhe. Ismail Omar Guelleh, Rais wa Jamhuri ya Djibouti, pia aliwasilisha Ripoti ya Maendeleo ya nchi hiyo kuhusu utekelezaji wa Programu yake ya Kitaifa ya Utekelezaji kwa Mapitio ya Msingi ya Jamhuri ya Djibouti. Mhe. Guelleh alibainisha kuwa serikali yake imechukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuridhia Eneo Huru la Biashara Barani Afrika ili kuboresha utawala nchini na kukuza utawala wa sheria.

26. 26. Djibouti pia imepiga hatua kubwa katika ulinzi wa watu walio katika mazingira magumu wakiwemo wanawake, watoto na watu wanaoishi na ulemavu. Programu ya maendeleo ya miundombinu ya barabara na bandari inaendelea vizuri, na juhudi hizo zitakuza

maendeleo ya sekta binafsi kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi. Kuanzishwa kwa Ofisi za Wataalamu wa Takwimu kulisifiwa kama utaratibu mzuri na pia hatua ya kuwaruhusu raia kupata huduma za hifadhi ya jamii

27. Rais alikaribisha ripoti hiyo akibainisha idadi kubwa ya ukosefu wa ajira na uhamiaji wa vijana kama baadhi ya vikwazo vinavyohitaji uingiliaji kati wa kimkakati
28. Mhe. Netumbo Nandi-Ndaitwah, Rais wa Jamhuri ya Namibia, pia aliwasilisha Ripoti ya Maendeleo kuhusu utekelezaji wa Ripoti ya Kitaifa ya Utekelezaji ya Mapitio Lengwa kuhusu ukosefu wa ajira kwa vijana iliyohitimishwa Desemba 2019.
29. Mhe. Nandi-Ndaitwah alikubali matokeo ya mapitio na akauhakikishia Mkutano Mkuu kwamba Namibia iko mbioni kutekeleza mapendekezo ya ripoti hiyo.
30. Alielezea hatua zifuatazo zilizochukuliwa hadi sasa ili kushughulikia ukosefu wa ajira kwa vijana:

    i. Kurekebisha mfumo wa elimu;

    ii. Kuimarisha mafunzo ya ufundi;

    iii. Kuanzishwa kwa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza;

    iv. Kuanzisha Mfuko wa Kitaifa wa Maendeleo ya Vijana

31. Mkutano huo ulimpongeza Mheshimiwa Chapo, Mheshimiwa Guelleh na Mheshimiwa Nandi-Ndaitwah kwa uongozi wao bora na juhudi zao thabiti za kuboresha utawala katika nchi zao. Mkutano huo ulithibitisha kikamilifu kwamba Mpango huo utaendelea kuiunga mkono Msumbiji, Djibouti, na Namibia katika kuimarisha utawala wa kidemokrasia.

32. Mhe. Dkt. William Ruto alisisitiza kujitolea kwake kwa dhati katika kuongoza uimarishaji wa taasisi za APRM katika uwezo wake kama Bingwa wa mageuzi ya taasisi za AU. Zaidi ya hayo, alijitolea kuongoza njia kwa kuharakisha utekelezaji wa vyombo vya APRM ya Kenya katika Sheria ya Bunge, kupitia mchakato unaoendelea sasa.

33. Mkutano huo ulitambua maendeleo makubwa yaliyopatikana katika kushushwa kwa APRM hadi ngazi ya chini ya kitaifa ya Kenya na azimio la serikali la kuwezesha mapitio ya pamoja, kupitia Mfumo wa Mapitio ya Pamoja wa Kaunti (CPRM) kwa kaunti 25 bora kati ya kaunti zote 47.

34. Zaidi ya hayo, Rais Ruto alitoa taarifa kwa Jukwaa kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika mchakato wa Mapitio Lengwa kuhusu Masuala ya Vijana na Ugatuzi na kuripoti kwamba Kenya ilikuwa mbioni kukamilisha mchakato huo kabla ya Mkutano wa 2027.

35. Mheshimiwa Sofiane Chaib, Mwenyekiti wa Kamati ya APR ya Wajumbe Maalum, aliwasilisha Ripoti ya Kamati hiyo kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 12 ya Katiba ya APRM na Kanuni za Utaratibu wa Jukwaa la APR na zile za Kamati ya Wajumbe Maalum

ya APR.

36. Mkutano huo uliidhinisha muundo wa Jukwaa la APR Troika kama ifuatavyo: Mwenyekiti: Jamhuri ya Uganda (2026-2028); Mwenyekiti Anayemaliza Muda wake: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria; Mwenyekiti Ajaye (2028-2030): Jamhuri ya Burundi.

37. Mkutano huo uliidhinisha kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa AU Wajumbe wapya 10 wa Jopo la Watu Mashuhuri wa APR kama ifuatavyo: Prof. Ben Abdallah Youcef (mwanaume): Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria (Afrika Kaskazini); Balozi. Soha Samir Nashid Gendi (mwanamke): Jamhuri ya Kiarabu ya Misri (Afrika Kaskazini); Dkt. Thelma Awori (mwanamke): Jamhuri ya Liberia (Afrika Magharibi); Dkt. Oluwakemi Adeola Obauelu (mwanamke): Shirikisho la Jamhuri ya Nigeria (Afrika Magharibi); Prof. Gilbert Maoundonodj (mwanaume): Jamhuri ya Chad (Afrika ya Kati); Prof. Désiré Manirakiza (kiume): Jamhuri ya Burundi (Afrika ya Kati); Balozi. Agnes Kalibala Kadama (mwanamke): Jamhuri ya Uganda (Afrika Mashariki); Prof. Olive Mugenda (mwanamke): Jamhuri ya Kenya (Afrika Mashariki); Dkt. Moeketsi Majoro (mwanaume): Ufalme wa Lesotho (Kusini mwa Afrika), na Balozi. Sibusiso Ndebele (mwanaume): Jamhuri ya Afrika Kusini (Kusini mwa Afrika).

38. Mkutano wa Wakuu wa Nchi uliidhinisha uteuzi wa Mkutano Mkuu wa AU wa Uongozi wa Jopo la Watu Mashuhuri la APR kama ifuatavyo: Mwenyekiti (2026): Prof. Olive Mugenda (mwanamke): Jamhuri ya Kenya (Afrika Mashariki); Makamu Mwenyekiti (2026) na Mwenyekiti Anayeingia (2027): Prof. Désiré Manirakiza (mwanaume): Jamhuri ya Burundi (Afrika ya Kati).

39. Mkutano huo ulitoa shukrani zake kubwa kwa Wajumbe wa Jopo la APR waliostaafu, Balozi Aly El-Hefny, Balozi Ali Ahmed Araita, Dkt. Abdoulie Janneh, Balozi Cherif Rahmani, Mheshimiwa Lydia Wanyoto-Mutende na Bw. Mathew Gowaseb kwa utumishi wao wa mfano wakati wa uongozi wao katika Jopo la Watu Mashuhuri la APR.

40. Mkutano huo uliidhinisha Ripoti ya Mwaka ya Sekretarieti ya APRM (2025-2026) na ulielezea kuridhika kwake na Mkurugenzi Mtendaji wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, Balozi. Marie-Antoinette Rose-Quatre, kwa maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa APRM 2025-2028 wenye matokeo yanayoonekana.

41. Mkutano ulipitisha Hitimisho la Mkutano wa 4 wa Pamoja wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika (PSC) na APRM uliofanyika kuanzia tarehe 7 hadi 8 Aprili 2025 mjini Johannesburg, Afrika Kusini na kuagiza taasisi hizo mbili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mapendekezo yake.

42. Mkutano huo uliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Sierra Leone kwa kufanikisha kuandaa Mkutano wa Tatu wa Ngazi ya Juu wa Afrika kuhusu Ushirikiano wa Kusini-Kusini na Pande ttatu kwa ajili ya Maendeleo Endelevu mjini Freetown kuanzia tarehe 7 hadi 9 Mei 2025. Mkutano huo uliidhinisha matokeo na mapendekezo ya Mkutano huo na kuzihimiza Nchi Wanachama na taasisi zote kuyatekeleza.

43. Mkutano huo uliipongeza Sekretarieti ya Bara ya APRM na wanachama wa Jukwaa la Mpango wa Utawala wa Afrika (AGA) kwa kufanikisha uzinduzi wa Ripoti ya Utawala wa Afrika 2025, ambayo inazingatia Utawala wa Maliasili, mwezi Julai 2025 mjini Accra, Jamhuri ya Ghana, pembezono mwa Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka, na pia kwa mipango iliyowekwa ili kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo yake. Mkutano huo uliipongeza zaidi Sekretarieti ya Bara ya APRM kwa kufanikisha uzinduzi wa Kanuni na Miongozo ya Afrika kuhusu Usimamizi wa Makampuni wakati wa Mkutano wa Tatu wa Ngazi ya Juu wa Afrika kuhusu Ushirikiano wa Kusini-Kusini na Pande tatu kwa Maendeleo Endelevu.

44. Mkutano uliidhinisha hitimisho la Kongamano la Vijana la APRM lililofanyika kuanzia tarehe 10 hadi 11 Desemba 2025 katika makao makuu ya Bunge la Afrika mjini Johannesburg, Jamhuri ya Afrika Kusini. Mkutano huo pia uliidhinisha kaulimbiu iliyopendekezwa kwa Ripoti ya Utawala wa Afrika 2027, kama ilivyopendekezwa na Jukwaa la AGA na Kongamano la Vijana la APRM, yaani: "*Vijana katika Utawala: Kutoka Ahadi hadi Ustawi*," na kuomba Sekretarieti ya Bara ya APRM, kwa kushirikiana na Jukwaa la AGA, kuanza maandalizi ya *Ripoti ya Utawala wa Afrika 2027* mara moja.

45. Mkutano huo ulitoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kuandaa kwa mafanikio Mkutano wa 4 wa Pamoja la PSC na APRM, pamoja na Mkutano wa 4 wa Vijana la APRM mjini Johannesburg.

46. Mkutano uliipongeza Sekretarieti ya Bara ya APRM kwa uwezeshaji bora wa mapitio ya nchi yaliyofanywa na Jopo la Watu Mashuhuri la APR, na utekelezaji wa utawala wa kielektroniki kama eneo la sita la mada ya utawala wa APRM.

47. Mkutano huo ulitoa shukrani zake zaidi kwa Sekretarieti ya Bara ya APRM kwa mipango iliyofanywa ili: kuhakikisha maandalizi ya Ripoti ya Utawala wa Afrika ya mwaka 2027; kusaidia Nchi Wanachama katika eneo la ukadiriaji wa mikopo na kuanzisha Shirika la Ukadiriaji wa Mikopo la Afrika; kuandaa *African Governance Series*; kuiweka APRM kama chombo bora cha tahadhari ya mapema kwa ajili ya kuzuia migogoro barani; kuendeleza Kielezo cha Utawala cha APRM; kuendeleza juhudi kuelekea utekelezaji wa Programu ya

Msaada wa Utawala wa APRM; na kuitisha mikutano yote ya kikatiba ya APRM kwa mujibu wa Katiba ya APRM na Kanuni za Uendeshaji.

48. Mkutano huo ulizingatia mipango iliyofanywa na Sekretarieti ya Bara ya APRM yenye lengo la kuhakikisha utekelezaji wa agizo la APRM kwa matokeo yanayoonekana, kama vile utafutaji wa rasilimali, ushirikiano, mawasiliano, utetezi na ufikiaji.

49. Mkutano ulikiri kwa kuridhika sana mchango wa hiari wa dola milioni moja (US$1,000,000 milioni 1) kutoka Algeria; mchango wa dola laki moja (US$100,000) kutoka Togo ka ajili malipo ya madeni yake kwa APRM; dola laki moja (US$100,000) kutoka Liberia kama malipo ya sehemu ya madeni yake; dola laki nne na thelathini na mbili (US$432,000) kutoka Senegal kama malipo kamili ya madeni yake, na ($500 015) kutoka Djibouti kwa ajili ya malipo ya madeni yake kwa APRM. Mkutano huo ulizitaka zaidi Nchi zingine wanachama wa APRM kulipa madeni yao yaliyosalia na kutoa michango ya hiari kwa APRM ili kuhakikisha umiliki kamili wa Mpango huo kwa Nchi wanachama wake.

50. Jamhuri ya Uganda iliahidi kuchangia kiasi cha dola 1,000,000 (dola milioni moja) wakati wa uongozi wake kama mwenyekiti wa APRM

51. Mkutano wa Wakuu wa Nchi ulisisitiza tena hitaji la kuimarisha uwezo wa APRM ili kutekeleza mamlaka yake iliyopanuliwa na kuimarisha uhuru wake wa kiutendaji. Pia ulisisitiza hitaji la APRM kupewa rasilimali watu wa kutosha na mgao wa bajeti ili kutekeleza mamlaka yake bila kizuizi.

52. Mkutano wa Wakuu wa Nchi pia unatoa shukrani zake za dhati kwa Mhe. Cyril Ramaphosa na Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kwa majengo mapya ya kipekee yaliyotolewa kwa Sekretarieti ya Bara ya APRM mjini Centurion, Pretoria, na kwa kuwa mwenyeji bora wa APRM nchini Afrika Kusini.

53. Mkutano huo ulimpongeza Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa uongozi wake mzuri wa APRM na kwa kuongoza kwa mfano wakati wa uongozi wake kama Mwenyekiti wa Jukwaa la APR. Hili lilionyeshwa, pamoja na mambo mengine, kupitia mchango wa hiari wa Algeria wa dola milioni moja (US$1,000,000); utekelezaji wa mapitio kamili ya nchi na mapitio manne lengwa; kujiunga kwa Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia kwenye APRM; na uimarishaji na uwekaji wa kimkakati wa APRM ili kutekeleza agizo lake kwa ajili ya matokeo yanayoonekana, hususani kupitia uundaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa APRM (2025–2028) kwa umakini mkubwa, pamoja na ukuzaji wa utawala bora kote barani.

54. Mkutano wa Wakuu wa Nchi ulimpongeza Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, kwa kuchaguliwa kwake kama Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakuu wa Nchi na Serikali la APR na kumhakikishia uungaji mkono kamili wa Jukwaa la APR.

55. Mkutano huo pia ulitoa shukrani zake kwa Wakuu wote wa Nchi na Serikali, Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU, vyombo vyote vya APRM na washirika kwa kufanya kazi bila kuchoka kuhakikisha kwamba APRM inatekeleza majukumu yake kwa ajili ya matokeo yanayoonekana.

56. Mkutano huo ulitoa shukrani zake kwa Wakuu wote wa Nchi na Serikali na wawakilishi wao, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Makamishna wa AU, Wajumbe wa Jopo la APR, Mkurugenzi Mtendaji wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, wanachama wa Jukwaa la AGA, Wakurugenzi Wakuu wa REC, Washirika na wageni waalikwa kwa kuhudhuria Mkutano wa 35 wa Kawaida wa Jukwaa la APR la Wakuu wa Nchi na Serikali.

57. Mkutano huo uliamua kwamba Mwenyekiti wa Jukwaa la APR, Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, angewasilisha Ripoti ya Matokeo ya Mkutano wa 35 wa APRM kwenye Mkutano wa 39 wa Kawaida wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU, uliopangwa kufanyika tarehe 14–15 Februari 2026, mjini Addis Ababa, Ethiopia, kwa ajili ya kujadiliwa na uwezekano wa kupitishwa.

58. Mkutano huo ulibainisha kwamba, kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya APRM, Maamuzi ya Mkutano Mkuu wa AU na kwa mujibu wa Kanuni za Uendeshaji za Jukwaa la APR, Mkutano wa 36 wa Kawaida wa Jukwaa la APR utafanyika pembezoni mwa Mkutano wa 40 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU, uliopangwa kufanyika Februari 2027, mjini Addis Ababa, Ethiopia.

**IMETOLEWA TAREHE 13 FEBRUARI 2026**

**ADDIS ABABA, JAMHURI YA SHIRIKISHO YA KIDEMOKRASIA YA ETHIOPIA**